



NAFASI ZA KAZI

Chama cha Walimu Tanzania (CWT) ni chama cha wafanyakazi katika kada ya walimu ambacho shughuli zake ni Tanzania Bara tu. Chama kimesajiliwa kwa Namba 004 chini ya Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Namba 6 ya Mwaka 2014. Chama cha Walimu Tanzania kina ofisi katika Wilaya na Mikoa yote ya Tanzania Bara. Ili kuboresha huduma kwa wanachama, CWT kinatangaza nafasi za ajira kwa watanzania walimu wenye sifa kujaza nafasi wazi za kazi zifuatazo:

1. KATIBU WA WILAYA – NAFASI 02

- (a) **Majukumu ya kazi:**
- Mtendaji mkuu wa shughuli za kila siku za chama katika ngazi ya wilaya.
 - Kuhakikisha kuwa walimu wanachama wanapata haki na maslahi yao kwa wakati kutoka kwa mwajiri.
 - Kutoa ushauri kwa walimu juu ya masuala mbalimbali yanayohusu ajira yao.
 - Kujenga uhusiano mzuri kati ya CWT na wadau mbalimbali wanaowahudumia walimu waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.
- (b) **Sifa za mwombaji:**
- Awe amesoma ualimu katika ngazi ya cheti na kuendelea.
 - Awe ni mwalimu mwanachama wa CWT na mwenye uzoefu wa masuala ya walimu na elimu nchini.
 - Awe ni mwajiriwa wa serikali na awe tayari kufanya kazi CWT kwa kibali cha likizo bila malipo kutoka serikalini.
 - Awe na ufahamu juu ya sheria za kazi zinazohusu utumishi wa umma haswa walimu.
 - Awe na leseni ya udereva na awe na uwezo wa kuendesha na kulitunza gari la chama.

NB. Walimu wanachama waliofanya usaili mwaka 2021 hawatakiwi kuomba tena.

2. MKUU WA IDARA YA WALIMU WENYE ULEMAVU: NAFASI 1

- (a) **Majukumu ya kazi:**
- Kusimamia utekelezaji wa sera ya CWT kuhusu walimu wenye ulemavu pamoja na sheria mbalimbali zinazohusu watu wenye ulemavu hasa walimu.
 - Kutoa huduma bora kwa walimu wenye ulemavu kulingana na miongozo ya CWT.
 - Kutambua mahitaji ya walimu wenye ulemavu kulingana na aina na kiwango cha ulemavu walio nao.
 - Kuhakikisha vikwazo vya utendaji wa kazi na mazingira wanayofanyia kazi walimu wenye Ulemavu vinaondolewa kwa kushauriana na kushirikiana na waajiri.
 - Kuimarisha ushirikiano na Vyama vya watu wenye Ulemavu, Taasisi na Mashirika yanayohudumia Watu wenye Ulemavu ndani na nje ya nchi.
 - Kujenga mazingira ya kujiamini kwa walimu wenye ulemavu kwa kuwapatia mafunzo mbalimbali ya kuwajengea uwezo mahali walipo.
 - Kuhakikisha kwamba Idara inakusanya na kutunza takwimu na taarifa sahihi za walimu wenye ulemavu.
 - Kufanya utafiti na kuandaa maandiko mradi ili kuweza kutatua changamoto za walimu wenye ulemavu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali.
 - Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na Katibu Mkuu.
- (b) **Sifa za mwombaji:**
- Awe ni Mwalimu mwanachama wa CWT mwenye elimu kuanzia Shahada ya Uzamili na kuendelea kutoka katika chuo kinachotambulika na serikali.
 - Awe na uwezo wa kufanya utafiti na kuandaa maandiko mradi ili kutambua na kutatua changamoto zinazohusu walimu wenye ulemavu.
 - Awe ni mwajiriwa wa serikali na awe tayari kufanya kazi CWT kwa kibali cha likizo bila malipo kutoka serikalini.
 - Awe na ufahamu juu ya sheria mbalimbali zinazohusu haki za watu wenye ulemavu.
 - Kuandaa mpango kazi, bajeti ya Idara pamoja na taarifa za kazi za robo mwaka, na mwaka mzima.

NB. Kipaumbele cha ajira kitatolewa kwa walimu wenye ulemavu.

MASHARTI YA JUMLA:

- Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania.
- Waombaji waambatanishe cheti cha kuzaliwa.
- Waombaji waambatanishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (detailed CV) yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu wa kuaminika.
- Maombi yote yaambatane na picha mbili (passport size) za rangi iliyoandikwa jina kwa nyuma, nakala ya vyeti vya kitaaluma na kitaalamu (academic and professional certificates).
- Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na TCU.
- Uwasilishaji wa taarifa za uwongo au za kughushi, wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.
- Maombi yanaweza kuandikwa kwa Kiswahili au kwa Kiingereza.
- Waombaji watakaokidhi vigezo ndio watakaoitwa kwenye usaili.
- Kwa nafasi ya makatibu wa Wilaya, maombi yatumwe kwa Makatibu wa Mikoa wa Chama cha Walimu Tanzania ambapo mwombaji anafanyia kazi.**
- Maombi ya nafasi ya Mkuu wa Idara ya Walimu wenye Ulemavu yatumwe moja kwa moja kwa **Katibu Mkuu, Chama cha Walimu Tanzania, S.L.P 3077, DODOMA.**
- Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 20 Aprili, 2023 saa 10.00 jioni.